## *Mwito ni mwaliko wa kuandaliwa kwa matumizi*

Ni wangapi wetu wanaweza kupanda ndege na kuondoka na mtu aliyeamua ana shauku na "mwito" wa kuwa rubani lakini hajawahi kupitia mafunzo halisi? Hivyo hivyo, ni wangapi wetu wanaweza kupanda meza ya upasuaji na kumruhusu mtu atufanyie upasuaji ambaye anahisi "ameitwa" kuwa daktari wa upasuaji? Jibu ni hili: Hakuna hata mmoja! Hata kutokana na msimamo wa kiasili tunaweza kujua zaidi kuliko kuaminia mambo ya uhai na mauti kwa wale ambao hawajitolei kujiandaa.

Hivyo hivyo ni kweli kutokana na msimamo wa kikristo. Tunapomjia Kristo na kuyatoa maisha yetu kwake, tunatarajia kupokea shauku zinazoelekeza maeneo ya huduma zetu ndani ya mwili wa Kristo. "Mwito" wetu ni mwaliko wa kutilia maanani wakati na fursa ambayo Mungu ametupa na kujiandaa kwa siku kuu za huduma. Ni wengi walioitwa lakini wachache wamechaguliwa. Pengine hii ni kwa sababu ya ukweli ya kuwa wachache tu ndio walioandaliwa kwa siku ya hitaji la Mungu. Jitolee katika kanisa lako na uanze kujiandaa leo.

*Ombi la leo*

Baba, nakushukuru ya kwamba kweli nimeitwa na Wewe. Nisaidie kujitolea mwito wangu kwako na kanisani mwangu, ili niwe nimeandaliwa vyema na kwa makini ninapotembea kueleka majira yangu kuu ya huduma.

*Maandiko ya Leo*

Mathayo 20:16 Yesu akamaliza kwa kusema, "Hivyo, walio wa mwisho watakuwa wa kwanza na wa kwanza watakuwa wa mwisho."

2 Petro 1:10 Kwa hiyo basi, ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi kuufanya huo wito wenu mlioitiwa na Mungu uwe jambo la kudumu katika maisha yenu; kama mkiishi namna hiyo hamtaanguka kamwe.

## *Usiruhusu moyo uliovunjika kukupa tumaini lililovunjika*

Katika maisha haya, tunaweza kukumbana na kuvunjika kwa moyo na hasara ambazo zinaweza kutuelekeza katika majonzi na kukata tamaa. Tunaelezea hii kama moyo uliovunjika. Wakati mazingira yetu yanaonekana kuwa duni, malengo yetu huwa katika kile kinachosababisha uchungu na kusahau taswira kuu – Mungu anatupenda, na amechukua usukani. Katika Marko Mtakatifu mlango wa 9, baba aliyevunjika moyo alimjia Yesu. Mwanawe alikuwa amepagawa na mapepo kwa miaka mingi. Yesu akasema, "Yote yawezekana ikiwa mtu anaamini." "Ninaamini," yule baba akasema.

“Lakini nisaidie kutoamini kwangu!” Huyu mtu alikuwa na tumaini ya kutosha iliyosalia kumuomba Yesu amsaidie.

Ikiwa umebeba mzigo mzito leo, usiruhusu moyo uliovunjika kukupa matumaini yaliyovunjika. Muombe Mungu akupe maono mema ya siku za usoni. Sasa, tembea ukielekea hiyo siku njema, ukiamini kuwa Atakupa nguvu na kukuhimiza katika safari. Kuna tumaini kwa kila moyo uliovunjika.

*Ombi la Leo*
Bwana, ninajua unaona ninachopitia siku ya leo. Ninaamini unanipenda na una lengo juu ya maisha yangu. Nisaidie kukutumainia zaidi, na kuona mbele ya wakati wangu wa uchungu. Asante kwa kuwa chanzo cha tumaini langu na amani.

*Maandiko ya Leo*
Zaburi 39:7 Na sasa ninangoja nini, Ee Bwana? Matumaini yangu ni kwako.

Yeremia 29:11 Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

## *Usipaze sauti kama hautajitokeza*

Wakati mmoja Yesu alisimulia hadithi kuhusu baba aliyekuwa na wana wawili. Baba yao akawauliza waje wafanye kazi naye siku fulani. Mmoja akakubali, na mwingine akakataa. Baadaye, aliyekataa akabadili nia na akaja kumtendea babaye kazi. Aliyekubali hakujitokeza.Yesu akauliza, “Ni nani aliyekuwa bora?”

Mungu, kama yule baba kwenye hadithi, anataka tuwe watoto wazuri, na analenga moyo wetu, sio tu kujitokeza kwetu. Msaada sio msaada hadi jambo zuri litendeke. Baba wetu wa mbinguni anangoja wanawe wajiunge naye katika kutenda kazi ya mavuno, kushiriki maisha yetu naye, na kupokea dhawabu anayotaka tushiriki naye. Usipaze sauti kama hautajitokeza.

*Ombi la Leo*
Baba, nataka kuwa mwana mwema. Nataka kukujua na kuwa na uhusiano mwema nawe. Kilicho cha muhimu kwako, ni cha muhimu kwangu pia. Tafadhali nionyeshe ninachoweza kutenda leo nikufurahishe Baba.

*Maandiko ya leo*
Zaburi 40:8 Kufanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu.

Yohana Mtakatifu 14:23 Yesu akamjibu, "Mtu akinipenda atashika neno langu, na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na kukaa naye.

Yohana Mtakatifu 17:3 Na uzima wa milele ndio huu: kukujua wewe uliye peke yako Mungu wa kweli, na kumjua Yesu Kristo uliyemtuma.

## ***Tumia rasilmali yako ya kiroho***

Watenda kazi wengine huelewa na kuchukua fursa ya kuweka rasilmali ya kustaafu. Wanafanya kazi kwa bidii, wakitenga kando kila juma, na kujenga rasilmali itakayotumika baadaye. Ufalme wa mbinguni unalinganishwa na mfano huu. Tunapoishi maisha ambaye Mungu anataka tuishi,tunapata hekima, kibali, na kuaminika. Hii ndiyo rasilimali yetu ya kiroho. Mara nyingi tunapata rasilimali ya kiroho zaidi ya matumizi yetu na tunatenga zisizotumiwa kwa matumizi ya baadaye.

Unaweza kutumia rasilmali yako ya kiroho kwa kuhimiza wengine kumtumikia Bwana ama kukupa kibali, ambacho kiatakuwa ni faida ya Ufalme. Mungu hutupa rasilamli ya kiroho zaidi ya tunavyohitaji. Tenga rasilmali zingine kufaidi wengine. Tumia rasilmali yako ya kiroho hapa duniani. Hautaihitaji mbinguni.

*Ombi la Leo*
Baba, ninataka kuwa mweka rasilmali mwema! Tafadhali, kwa uwezo wa Roho Wako Mtakatifu, nionyeshe jinsi nitakavyotumia vyema kila fursa unayonipa. Nisaidie kujua wakati na kiwango nitakacho hifadhi kwa wengine. Kila nilichonacho ni Chako.

*Maandiko ya Leo*
Yohana Mtakatifu 9:4 Kukiwa bado mchana yatupasa kuendelea kufanya kazi za yule aliyenituma; maana usiku unakuja ambapo mtu hawezi kufanya kazi.

Waefeso 5:16 Tumieni vizuri muda mlio nao maana siku hizi ni mbaya.

## ***Sio yule afikaye juu kwanza anaye maanisha.***

Katika jamii yetu inayoshindana, sisi hutilia mkazo wa kufaulu kwa kufika juu kwanza. Na matokeo yake wakuu wa mashirika wamejitoa

mhanga umuhimu wao katika mathabahu ya tamaa. Wamekosa umuhimu wa ukweli jinsi safari anavyo ongozwa ni muhimu kuliko safari yenyewe. Tunapo maliza hua sio muhimu kama kumaliza tukiwa bado na tabia zetu. Wengi ambao hufika kileleni juu baadaye huanguka kwa sababu safari yao kuelekea juu ilikuwa ya makato na amuzi ambazo hazikufaa ambazo ziliwagharimu kuliko vile walivyokuwa wamehesabu.

Je wewe? Kiburi chako na tamaa yako isio na mwelekeo ndiyo imekupandisha juu kwa kasi ukitumia mafuta ya undanganyifu? Chukua hesabu yam bio zako za kibinafsi na utengeneze mapito yako na ushujaa, uadilifu, uvumilivu, na kuto kata tamaa. Tumia wakati wako kumsaidia mtu mwingine afaulu pia. Chukua hatua zilizo na umakini na ufanye uamuzi wa kiungu ili utakapofika kileleni, ukae pale.

*Ombi la leo*

Baba nisaidie leo nitazame kwa uangalifu jinsi ninavyokimbia riadha yangu. Sitaamini imani mbaya ya kwamba kufika pale wa kwanza ina maana mimi ndiye bora zaidi. Tafadhali nisaidie kuelekeza maisha yangu katika nyanja zote, kulingana na Neno Lako.

*Masomo ya leo:*

Mathayo 19:30; Lakini walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.

Mathayo 6:33; Bali, zingatieni kwanza Ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada.

## ***Ufanisi wa kweli utazikaza shani zako***

Jambo moja ni hakika maishani- ili kukua kiroho, kiasili, kimawazo, na kwa kiuhusiano na wengine, lazima tukubali kulipa gharama. Kama vile mwili wa kiasili utapatwa na njaa usipo pata lishe bora, hivyo ndivyo ilivyo katika kila hali ya maisha. Hatuwezi kua ama kuendelea maishani bila kuelewa kwanza ya kwamba lazima tutumie kile tulicho nacho ili tupate kitu tunacho kitamani.

Jinsi maisha yanavyoendelea baadhi ya shani tutakavyohitaji kutumia huenda ikawa ni fedha zetu, wakati wetu, ama mapenzi yetu kwa njia isyokuwa ya ubinafsi. Labda itahusisha kuacha kiburi chetu na kumsamehea mtu ambaye ametuumiza. Ufanisi wa kweli utakuwa na gharama yake kwa mambo yako. Kuwa tayari kukazwa Mungu anapo anza kukutumia zaidi.

*Ombi la leo*

Ewe Mungu, nisaidie nikubali kukaza na kutumia shani zangu ili niweze kukua maishani. Nipe hakima, ufambanuzi, na hasa tama zaidi yakufikia juu zaidi kwa kiwango cha juu ndani Yako.

*Masomo ya leo:*

Wafilipi3:12; si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.

2 Samueli 24:24; lakini mfalme akamwambia Arauna, La, sivyo; lakini kweli nitavinunua kwako kwa dhamana yake; wala sitamtolea BWANA Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizogharimia.

## ***Maisha yetu yapaswa kuwa ni andiko ambalo ni Mungu pakee aweza kuandika.***

Wakati tunapeana maisha yetu kwa Kristo, yeye hufunika dhambi zetu zote. Mambo yote ya kale hupita na mambo yote hufanyika upya. Uwezo wote hufanyika mwingi zaidi ya mawazo au ufahamu wetu. Maisha yetu katika mikono yake Bwana imepangwa ijae mambo ya kushangaza, mara nyingi tunzo, na ufanisi uliojaa changa moto ambazo zinatupa sisi kila fursa ya kukua.

Kile kinaonekana kama chakushangaza kwetu mara nyingi huwa ni mpango wa Mungu. Hata hivyo, maisha yetu yafaa kuwa ni andiko ambalo ni Mungu pekee aweza kuandika na haandiki kimakosa. Kwa hivyo, yaweke maisha yako kwa mokino ya Mungu na usifadhaike wakati mambo ambayo haukutarajia, hayakufaa kukutendekea, na hauwezi kufikiria yanapokuja kwa njia yako. Imini Mungu na uendelee kuishi andiko analoliandika kwa ushindi wako. Yeye yuko kwa usukani

*Ombi la leo*

Baba, asante sana kwa kuuondoa uchafu wote wangu wa kale maishani mwangu. Inanipa mimi siku mpya,fursa mpya, tumaini mpya, na usoni mpya. Ninatamani kwa upendo Uandike kurasa za maisha yangu leo na milele.

*Masomo ya leo:*

1 wakorinitho 7:23; Nyote mmenunuliwa kwa bei; kwa hiyo msiwe tena watumwa wa watu.

Waebrania 5:9; Na alipofanywa mkamilifu, akawa chanzo cha wokovu wa milele kwa wale wote wanaomtii,

Mariko 11:22; Yesu akawaambia, "Mwaminini Mungu.

## ***Weka kichwa chako ndani ya mashindano, roho yako ndani ya mashindano, na mikono yako ndani ya mashindano***

Ili upate ushindi kwa mashindano yoyote ama upate jambo lolote kuu maishani, lazima tufanye kwa umakini na kujitolea. Kujaribu na moyo nusu ama umakini uliogawanywa utazaa mazao nusu. Kama msemo unavyosemwa, chochote mtu anachofanya, ni vyema kifanywa inavyopaswa. Kutenda kitu kwa njia inayofaa inabainisha ujumuisho wa mawazo, roho, na matendo.

Kama maumbile ya Mungu, tunatenda bora zaidi kwa kutumia kila kiungo cha utatu wetu( mwili, roho na nafsi) kwa kuelewana kwa hali ya juu iwezekanavyo kuelekea kwa lengo letu na mwito wetu. Kuweka kichwa, roho, na mikono ndani ya mashindano, itatupatia ushindi. Unapeana yako 'yote' kwa mwito wako wa sasa na ndoto zako za usoni?

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie leo kutumia mimi wote kukutumikia Wewe wote. Nisaidie kujua ya kwamba chochote ninachotamani kufaulu ndani yake kitagharimu kutia kichwa changu, roho yangu, na mikono yangu. Nifunze njia zako, ewe Bwana.

*Masomo ya leo:*

1 wathesolenike 5:23; Mungu anayetupatia amani awafanye ninyi watakatifu kwa kila namna na kuzilinda nafsi zenu--roho, mioyo na miili yenu--mbali na hatia yoyote wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.

Kumukumbu La Torati 11:18; kwa hiyo yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu.

2 Samueli 6:14; Daudi akacheza mbele za Bwana kwa nguvu zake zote; na Daudi alikuwa amevaa naivera ya kitani

## ***Usiwahi mwamini kabisa mwanadamu asiyetembea kwa kuchuchuma***

Kwa kumfuata kiongozi, kutafuata ushauri, ama kunyenyekea chini ya kiongozi ama muelekezi, tunafaa kuwa na tamaa ya kujua ujuzi wao wa maisha na pia kuhitimu kwao kwa kielimu. Mafunzo yafunzwayo ndani ya darasa la maisha mara nyingi humfanya mtu kuwa anayotosha na kufaa kuwa na wafuasi.

Katika kutembea kwetu na Kristo, tutakuwa na msimu wa kusikiza Neno, na pia wakati wa majaribu na mateso. Nyakati hizi huweka Neno ambalo tumejifunza katika matendo. Imani itajaribiwa ili itupe ujuzi wakueleweka kwa kila mwanafunzi wa Neno la Mungu. Mitihani hufanyika ushuhuda tunapotumia mambo tuliyojifunza kwa hali za kimaisha. Mara nyingi,ming'ang'ano na alama za majeruhi yanayotokana na haya hutumika kwa kutupa sisi nguvu, na uadilifu na wakati mwingi kuvunjika tulikokuhitaji ili tuuende maisha yetu kuwa sawasawa. Alama hizi za vita hufanyika vipaji vya ushindi wetu.

### *Ombi la leo*

Ahsante Mungu kwa fursa ya kukufahamu kupitia kujaribiwa na mateso. Hebu maisha yangu yang'ae na ushuhuda wa wema Wako na Uaminifu Wako.

### *Masomo ya leo:*

2 wakorinitho 2:14; Lakini, shukrani kwa Mungu anayetuongoza daima katika msafara wa ushindi wa Kristo. Yeye hutufanya tuueneze ukweli wa Kristo kama harufu nzuri, kila mahali.

Mwanzo 32:25; naye alipoona ya kuwa hamshindi, alimgusa panapo uvungu wa paja lake; ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye.

1 Wakorinitho 15:57 Lakini tumshukuru Mungu anayetupatia ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

## *Yesu hutuokoa kutokana na umilele ndani jehanamu na jehanamu ya maisha haya*

Kwa kufanya uamuzi mfagisi mmoja kwa Kristo tunakumbatia umilele na Yeye. Hata hivyo, ni tamaa Yako kutotuokoa kwa umilele ndani ya jehanamu pakee lakini pia kutuokoa kutoka kwa jehanamu ya maisha haya. Lazima tuzaliwe tena na baadaye, kila mmoja wetu inabidi ajifunze kuishi kwa ujuzi wa mtu aliyezaliwa mara ya pili kwa kutumia Neno Lake kwa maisha yetu ya kila siku.

Je na wewe? Unaruhusu nguvu za Neno la Mungu kubadilisha maisha yako ya sasa na pia ya usoni? Unatafuta na baadaye kunyenyekea chini ya Neno la Mungu liishilo kama mamlaka yako ya mwisho, hata kama inaonekana kama ni gumu? Usiepuke pekee umilele wa jehanamu, lakini epuka umilele wa maisha haya kwa kutii Neno la Mungu.

*Ombi la leo:*

Ahsante Mungu kwa anjili ya nyumbani mwangu mwa umilele. Nakushukuru pia kwa kunipea maagizo ya kila siku kutokana na Neno Lako ambayo yataniokoa na vita zote, majaribu, na mitihani ya maisha haya. Nisaidie kuamini na kutii kila siku ili niwe na amani kwa maisha haya na maisha yajayo.

*Masomo ya leo:*

1 Yohana 3:22; na twaweza kupokea kwake chochote tunachoomba, maana tunazitii amri zake na kufanya yale yanayompendeza.

Marko 10:29-30; Yesu akasema, "Kweli nawaambieni, kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu, au dada, au mama, au baba, au watoto au mashamba kwa ajili yangu na kwa ajili ya Habari Njema, atapokea mara mia zaidi wakati huu wa sasa nyumba, ndugu, dada, mama, watoto na mashamba pamoja na mateso; na katika wakati ujao atapokea uzima wa milele.

## *Mashetani wote ni waongo lakini sio waongo wote mashetani*

Shetani ni muongo. Bibilia inasema yeye ni baba ya uongo. Yeye ndiye mwanzo na mwisho wa uongo. Nguvu zile kubwa ambazo shetani hutumia ni undanganyifu. Uepo wake wote unamsingi wa kujaribu kutufanya tuamini uongo, kwamba maisha yetu yaweza kuwa mazuri

bila Yesu. Yeye hutumia watu, hali, mambo na tama yetu kujilinda tusiwe wakutumiwa kueneza uongo huu.

Udhaifu mmoja mkubwa wa shetani ni kuwa hajakuona kwa udhamana wako wote. Anaona kwamba utakubaliana kwa urahisi. Lakini kuna Roho mkubwa ndani yetu. Labda sisi sio wakamilifu lakini mwelekeo wote ni wa ukamilifu. Waweza fanya dhambi ama unene maneno ya undanganyifu, yanayoelekezwa kwa kubadilisha like msikizaji anacho amini, ama unaweza kusema uongo ulio wazi. Hii haikufanyi uwe shetani lakini inakufanya utende kama Yeye. Wacha kundanganya na uulize Mungu akusamehee. Sema ukweli kwa njia ya upendo ama usiseme kitu chochote.

*Ombi la leo:*

Baba, tafadhali nikumbushe niseme ukweli wakati wote. Nisaidie nikuamini Wewe kwa kunishughulikia badala ya mimi kutumia njia ya uongo kujishughulikia mwenyewe kwa undanganyifu. Mimi nimejitoa Kwako na sitaamini uongo wa adui kwamba maisha yangu yaweza kuwa mazuri bila Yesu.

*Masomo ya leo:*

Waefeso 4:15; Ila, sisi tukisema ukweli kwa moyo wa mapendo tutakua zidi katika kila jambo kulingana na Kristo ambaye ndiye kichwa;

Yohana 8:44; Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi na mnataka tu kutekeleza tamaa za baba yenu. Yeye alikuwa muuaji tangu mwanzo; hana msimamo katika ukweli, kwani ukweli haumo ndani yake. Kila asemapo uongo, husema kutokana na hali yake ya maumbile, maana yeye ni mwongo na baba wa uongo.

## ***Bainisha kati ya Saluli wako na Goliathi***

Daudi alikuwa na maadui wawili wa ukweli maishani mwako na aliwachukulia kwa utofauti. Adui mmoja, Mfalme Sauli, alimfuata miaka mingi akijaribu kumuua na aharibu siku za usoni mwako uliokuwa umepakwa mafuta. Kisha kuna Magoliathi wa maisha ambao hutusumbua na kutuchanga moto. Ni kopi kina wafanya maadui hawa kuwa tofauti? Mfalme Sauli ingawa alikuwa hatari kwa Daudi, alikuwa ni mtu ambaye ni Mungu aliweka katika maisha ya Daudi na Daudi alikuwa chini ya mamlaka ya Sauli. Ni Mungu pekee anebadilisha haya. Daudi hangeinua mkono wake mwenyewe dhidi ya mamlaka yake. Goliathi hata hivyo, hakuwa katika hali nyingine yoyote ila alikuwa tu ni

adui wa Daudi. Ilikuwa ni haki ya Daudi na wajibu wake kusimama kinyume na Goliathi ili awezeshe kumshinda.

Kati ya maadui wawili maishani mwako, ni wagani Mfalme Sauli ambaye lazima Mungu akuondolee na ni wagani Magoliathi ambao lazima wewe ung'ang'ane nao na usimame kinyume nao?

*Ombi la leo:*

Ba ba, ninakupenda. Tafadhali nisaidie niwe na tabia nzuri ya kuheshimu na kuamini uongozi ulioko ndani ya maisha yangu. Hata wakijaribu kuniondoa, usiniruhusu kuchukua hili jambo isivyofaa. Bwana, nisaidie kuwaharibu Magoriathi wa maisha yangu ambao hunitukana na kunilaani mimi, watu Wako, na Wewe. Ahsante kwa nguvu zako za ushindi.

*Maandiko ya leo:*

I Samueli 24:6; Akawaambia watu wake,Hasha! Nisimtendee Bwana wangu, masihi wa BWANA, neno hili kuunyosha mkono wangu juu yake, kwa maana yeye ni Masihi wa BWANA.

1 Samueli 17:46; siku hii ya leo BWANA atakuua mikononi mwangu nami nitakupiga, nakukuondolea kichwa chako nami leo nitawapa ndege wa angani na wanyama wan chi mizoga ya majeshi Wafilisti, ili kwamba dnia nzima wajue kuwa yuko Mungu katika Isiraeli.

## ***Enenda kwa amani usienende ukiwa vipande***

Mungu hutupea sisi kila fursa ya kumuitia Yeye na kumjia bila kujalisha hali tunazokumbana nazo. Tulimuita Mungu, atatusikia, atatujibu, na atatuonyesha mambo makuu ya ajabu tusiyo yajua. Ana jawabu kwa shida zetu zote na masumbuko yetu yote ya maisha. Kumuita yeye na kuja kwa uwepo Wake na malilio na sifa zetu humfanya atusikie. Katika uwepo Wake kuna furaha tele. Hata hivyo, hatuwezi kudumu kila wakati katika chumba chetu cha maombi tukilowa kwa upendo Wake, starehe Yake, na neema Yake. Wakati hufika ili tuweze kuendelea na kukumbana na hali za maisha.

Katika nyakati hizi, ni tumaini lake Mungu kwamba tuenende kwa amani sio tukiwa vipande. Wacha amani ya Bwana ipatikanayo kwa maombi, itembee nawewe ndani ya shighuli za kila siku ya maisha.

*Ombi la leo:*

Baba ahasante kwa amani katika hali zote. Nakutazamia kunionyesha mipango Yako kwa maisha yangu. Nisaidie nifanye vyema iwezekanavyo katika kila hali ya maisha ninapotembea katika amani Yako.

*Maandiko ya leo:*

Wafilipi 4:7; na amani ya Mungu, upitao ufahamu wote wa wanadamu, iwe na roho zenu na nia yenu katika Kristo Yesu.

Wafilipi 4:9; mambo hayo ambayo umejifunza, na kupokea, na kusikia na kuona ndani yangu, fanya; na Mungu wa amani atakuwa na wewe.

Wakolosai 3:15; Nayo amani ya Kristo itawale mioyoni mwenu; maana kwa ajili hiyo ninyi mmeitwa katika mwili huo mmoja. Tena muwe na shukrani!

## ***Mungu hupenda uhai, lakini ameruhusu uamuzi***

Ulijua amuzi ulizofanya jana tayari zimepata matokeo katika maisha yako na siku zako za usoni? Unaishi leo uamuzi uliofanya jana. Aaah, kanuni aina gani! Naweza badilisha siku zangu za kesho? Ndiyo! Mungu anataka tuwe na maisha ya kupendeza inavyowezekana, lakini hayo maisha lazima yatembewe katika njia Zake wala sio njia zetu, katika amuzi Zake wala sio zetu.

Tunapoamua kufanya amuzi kulingana na hali zetu ama kila kinaweza tupa starehe, basi yale bora ya Mungu kwa maisha yetu huenda tusiyafikie. Jaribu kutoafanya amuzi zinazokufaa, ila zilizoshawishika na zinazoongeza tabia kwa maisha yako kuliko zisizoeleweka. Mungu hupenda uhai… Yeye ako pale kwa sababu ya maisha yako… lakini anaturuhusu uamuzi wetu.

*Ombi la leo:*

Mungu tafadhali nisaidie kufanya amuzi zenye manufaa leo ambazo zitabainisha kesho yangu ndani ya hatima ambayo umeunda kwa sababu yangu. Nataka nifanane nawe zaidi. Nifanye niwe kama umbo la Mwanao Mpendwa. Nachagua Uhai!

*Maandiko ya leo:*

Yoshua 24:15; nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakaye mtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo

baba zenu waliitumikia ng'ambo yam to au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.

Isaya 7:14-15; kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara tazama, bikira ataichukua mamba, atazaa mtoto mwanamme, naye atamwita jina lake Imanueli. Siagi na asali atakula,wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema.

Yoeli 3:14; makutano makubwa, makutano makubwa, wamo katika bonde la kukata maneno! Kwa maana siku ya Bwana i karibu katika bonde la kukata maneno.

## *Kanisa imejumuisha wenye kuhudhulia, wenye kukaa, wenye kuomba, na wenye kulipa... umeitwa kutumika wapi?*

Ili hata mchezo wa mpira ufaulu, inagharimu kila mtu kuwa mahali pake, ni zaidi aina gani katika vita kati ya nguvu za Mungu na za shetani kuhusu nafsi ya wanadamu? Kanisa sio jamii ya Mungu, mwili na bibi arusi wa Kristo pekee, lakini pia ni jeshi la Mungu duniani.

Kanisa ni kusanyiko la Wakristo walioitwa pamoja na kutengwa, kila mmoja wao ana wajibu wa kufanya juhudi hizi zifaulu. Tumejimuishwa kwa wale wataenda na kusema, wale watakaa pale kwa kazi, wale wataombea jambo hili, na wale watatoa fedha kugharamia kampeni. Ni nini Mungu amekuita kufanya? Chukua nafasi yako... hebu twende,hebu tupigane, hebu tupate ushindi!

### *Ombi la leo:*

Mungu, naamua kufanya nafasi yangu kwa ajili ya Ufalme Wako na kwa sababu ya Kristo. Nionyeshe nimeitwa kwa sababu gani, niandae na unitumie, ewe Bwana. Mimi niwako uniamurishe.

### *Maandiko ya leo:*

Warumi 12:4; Mwili una viungo vingi, kila kimoja na kazi yake.

1 wakorinitho 12:12; Kama vile mwili ulivyo mmoja wenye viungo vingi, na viungo hivyo vyote--ingawaje ni vingi--hufanya mwili mmoja, ndivyo ilivyo pia kwa Kristo.

Waefeso 4:16; chini ya uongozi wake, viungo vyote vya mwili hushikamana pamoja, na mwili wote hutegemezwa kwa msaada wa viungo vyake. Basi, kila kiungo kikitekeleza kazi yake ipasavyo, mwili wote hukua na kujijenga katika upendo.

## ***Aliyesahihi sio muhimu kama kilicho sahihi***

Wakati mwingine tukiwa kwa mazungumzo na mtu mwingine, kuzungumza kwetu hubainishwa na tama zetu za kibinafsi. Kwa ukawaida, mawazo yetu na matamko yetu huegemea kile kibora kwa sababu yetu na kinachoweza kutuwezesha kuboresha dondoo letu. Kila mtu huwa sahihi machoni mwake mwenyewe. Hata hivyo, sio kila mtu aliye sawa. Kupanua kuelewa kwako, jaribu mtihani huu. Wakati utakuwa na kutoelewana kwa mazungumzo na mtu mwingine, uliza huyo mtu mbadilishane pande kwa mda kidogo. Yeye aongee kwa niaba yako nawe kwa niaba yake.

Jaribio hili laweza kuwa na mafunzo ama la kutisha. Kwa wale wako kwa hali nzuri kiasi kwamba waweza kujaribu kutafuta uamuzi mzuri kabisa, kuanzia mitazamo isiyokubaliana inaweza kuwa chanzo zha dhamana cha kupata ufahamu na kusuluhisha matatizo.  Mng'ang'ano mara nyingi huwa ni hatua muhimu ya umoja.

### *Ombi la leo:*

Baba tafadhali nisaidie kuchukua maoni ya watu wengine na umuhimu kama ninavyochukua yangu pia. Nipe neema ya kuwaheshimu wale wasiokubaliana na mimi na ujuzi wa kuafikia uamuzi ule unaofaa kwa watu wote wanaohusika. Nionyeshe ukweli wako kupitia macho yangu na macho yaw engine.

### *Maandiko ya leo:*

Isaya 1:18; 'haya, njoni, tusemezane,' asema Bwana. 'Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu'

Matendo ya mitume 11:17; Basi, kama Mungu amewapa pia watu wa mataifa mengine zawadi ileile aliyotupa sisi tulipomwamini Bwana Yesu Kristo, je, mimi ni nani hata nijaribu kumpinga Mungu?"

Wagalatia 2:11; Lakini Kefa alipofika Antiokia nilimpinga waziwazi maana alikuwa amekosea.

## *Kusanyiko ambalo sio la waijilisti mara nyingi huwa wala watu*

Amri pekee ambayo Mungu alipea kanisa ilikuwa kuenda dunia nzima wakihubiri Uzuri wa Mungu na kuwafanya wafuasi. Yesu akasema alikuja pekee kutafuta na kuokoa waliopotea na aliwaacha bila kujali wale kondoo 99 waliokoka tayari na wanaolekea mbinguni kuishi milele kuenda nje kumtafuta mmoja aliyekuwa amepotea. Ni wazi kwamba tumeitwa kupeleka ujumbe wa injili wakukomboa nafsi, mashahidi wa injili ya upendo wa Kristo Yesu.  Wanaowachilia hili jukumu la kimsingi wanaweza kuwa wamepeana haki yao yakuitwa kanisa.

Makanisa mengi hugawanyika na kuachana juu ya shida ndogo ndogo na shida za kidunia kama vile  rangi na mkeka , uamuzi wa nyimbo ama ni nani atakayeongoza mchezo wa Krismasi. Wakati huu, nafsi zinapotezwa na zinakufa zikielekea jehanamu wakati kanisa linabishana, likiumana na kukulana. Umbea na mvutano hazina nafasi ndani ya nyumba ya Mungu. Usiwe mtu wa masengenyo.

*<u>Ombi la leo:</u>*

Ewe Bwana, naomba unipe mimi na wengine ninaoshiriki nao hisia njema ya kutobishana kuhusu mambo yasiyo na umuhimu na yyasiyo na uwezo wakuokoa nafsi kwa ufalme Wako. Nitaamua kupitia mapito ya juu ya kujukumika.

*<u>Maandiko ya leo:</u>*

1 Timotheo5:13; Wajane kama hao huanza kupoteza wakati wao wakizurura nyumba hata nyumba; tena ubaya zaidi ni kwamba huanza kuwasengenya watu, na kujitia katika mambo ya watu wengine, huku wakisema mambo ambayo hawangepaswa kusema.

2 Wathesolonike 3:11; Tunasema mambo hayo kwa sababu tumesikia kwamba wako baadhi yenu ambao ni wavivu na ambao hawafanyi chochote, isipokuwa tu kujiingiza katika mambo ya watu wengine.

Mithali 11:30; tunda la haki ni mti wa uzima, na anayeokoa nafsi ana hekima.

## *Ushindi maishani hufanyika siku moja baada ya nyingine*

Mabingwa hawazaliwi, wanakuzwa baada ya msimu. Wamebainisha malengo yao kwa uwazi. Wanajua kile wanataka kupata maishani. Washindi wengi wa medali za dhahabu katika riadha, walianza kuwazia jinsi ya kushinda ushindi huu wa kifahari miaka kadhaa kabla waanze kuhitimu kuhusika.

Umewahi kuota ukiwa bora zaidi… mme mzuri zaidi, mke, baba, mama, mwana wa kiume, binti ama mtoto wa Mungu aliye bora zaidi inavyowezekana? Yote huanzia kwa shauku. Kisha inalazimu uchukue kila siku na uwe na mpango Fulani wakufanyika mkuu. Mazoezi ndiyo yanayotenganisha washindi na wale wa kujaribu. Unaona, ushindi maishani ni siku moja baada ya nyingine. Hautawahi fanyika bingwa maishani hadi ujifunze kupata ushindi wa kila siku.

*Ombi la leo:*

B aba, naomba unisaidie kuwa na maono ya siku za usoni na mpango wa kila siku. Niwezeshe kutazamia kesho bila kutoa dhabihu siku yangu ya leo. Nikumbushe kufanya mambo madogo ili Uniamini na mambo makubwa. Nahitaji msaada wako kufanyika bora jinsi iwezekanavyo.

*Maandiko ya leo:*

1 Wakorinitho 9:24; Je, hamjui kwamba katika uwanja wa michezo, ingawa wapiga mbio wote hukimbia, ni mmoja tu anayejinyakulia zawadi?

Waebrania 12:1; Sisi tunalo kundi hili kubwa la mashahidi mbele yetu. Kwa hiyo tuondoe kila kizuizi kinachotuzuia, na dhambi ile inayotung`ang`ania. Tupige mbio kwa uvumilivu katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu.

## *Usisahau kubeba chakula cha saa saba.*

Leo, Yesu anainua macho yake na anaona kikundi kikubwa kikimjia. Anatuuliza kama tutaweza kupata Mkate wa Uzima wa kikundi kikubwa namna hii. Yesu tayari anajua jibu la swali Lake. Hata hivyo, anatarajia tuwape kusanyiko Mkate wa Uzima. Kama waijua hadithi katika Mariko 6, wanafunzi hawakujua wafanye nini. Walikuwa hawajajiandaa kwa ajili ya siku yao na hawakuwa wameona umuhimu wa kubeba chakula cha mchana.

Kidogo ni kingi kwa mkono wa Bwana, na mambomadogo tunayoweza kumpea Yeye kila siku yaweza kufanya utofauti mkubwa. Kijana mmoja alikuwa amechukuwa wakati na kijiandaa hiyo siku. Kama matokeo,

Yesu alichukua mahitaji haya ya kibinafsi na kuyajumuisha kulisha maelfu waliokuwa hawajajiandaa. Usisahau kubeba chakula cha mchana. Chukuwa wakati wako kila asubuhi kusikiza Neno la Mungu na ulibebe popote utakapoenda.

*Ombi la leo:*

Baba ahsante kwa vile mimi ni mwana wa nidhamu. Ninafurahia kujiandaa kwa sababu ya siku zangu za usoni. Nitaanza leo kujiandaa ili niwe tayari Ukiniita. Tumia kidogo nilicho nacho kulisha kusanyiko. Niko huru.

*Maandiko ya leo:*

Yohana 6:5; Basi, Yesu na alipotazama na kuona umati wa watu ukija kwake, alimwambia Filipo, "Tununue wapi mikate ili watu hawa wapate kula?"

Yohana 6:9; Yupo hapa mtoto mmoja aliye na mikate mitano ya shayiri na samaki wawili; lakini hivi vyatosha nini kwa watu wengi kama hawa?"

## *Kumbatia utamaduni wa Kifalme.*

Dunia nzima, kila taifa, na hata, makundi mengi yamejaa wingi wa watu kutoka kwa mila mbalimbali, makabila, na tamanduni. Kila moja yapo inafurahia urithi na historia ilioachwa na mababu aliopeana mila na desturi aina hizi kwa kila kundi. Mila yetu san asana inatuonyesha ni kipi sahihi na ni lipi makosa, ile inakubalika na isiyokubalika, na inatupea jukwa la kila kundi la watu wanaoelewana kuweka sheria za maisha, ili tuishi vizuri na inavyokubalika na wengine ndani ya kundi letu.

Mila yetu haituunganishi na watu peke yake lakini, inatugawanya pia kutokana na wale wasiokumbatia imani yote ya pamoja na tabia za maisha. Kinachokubalika kwa mila hii chaweza kuwa chukizo kwa nyingine. Ni kwa sababu hiyo sisi kama waumini wa Kristo na washirika wa kanisalazima tukumbatie mila za Ufalme wa Mungu kuliko zetu za tuliko zaliwa. Lazima tujikaze tuweke utu wetu wa kale na tujivishe na utu mpya, wananchi wa mbinguni na mwana wa Mungu. Kumbatia utamaduni wa Kifalme.

*Ombi la leo:*

Baba, nifunze njia Zako ninapokazana kukumbatia mila na desturi za Ufalme Wako zaidi ya zile zangu. Nisaidie nibadilike pale panahitaji kubadilika katika jina la Yesu.

*Maandiko ya leo:*

Mathayo Mtakatifu 18:3; kisha akasema, "Nawaambieni kweli, msipogeuka na kuwa kama watoto, hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni.

Waefeso 3:20; Kwake yeye ambaye kwa nguvu yake ifanyayo kazi ndani yetu, aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria;

Waefeso 2:19; Basi, ninyi si wageni tena, wala si watu wa nje; ninyi ni raia pamoja na watu wa Mungu, na ni watu wa jamaa ya Mungu.

Hatuwezi panga uhusiano na Mungu

Mungu ni Mungu wa maono zaidi ya mafikira yetu, zaidi ya mipango yetu, na mara nyingi zaidi ya uwezo wetu kuweka mpango Wako kupitia kumanisha kwa sawa lakini usimamizi wa kimpangilio. Hatima haidhibitishwi kwa kuinua mikono na kutimizwa kwa mipango ya Mungu kuko juu zaidi ya uwezo wa mwanadamu. Njia zake ziko mbali hatuwezi kusijua. Kwa sababu hii, kila mtu binafsi, kila jamii, na mambo yote yanayoihusu kanisa, yafaa kuwa na mwongozo wa Kiroho sio kuongozwa kwa mpango wa kidemokrasia.

Mungu sio mwenye  kutowazia. Hata hivyo, Yeye ni mkubwa  kuliko mawazo ya mwanadamu na hayamzuii chochote. Haijalishi aliye nafasi ya pili ni nani mradi Mungu yuko nafasi ya kwanza. Watu ama kanisa lisipojali ni nani atanufaika, waweza kufanya mambo yasio na mipaka.

*Ombi la leo:*

Mungu, niongoze kwa roho Wako na unipe neema na ujasiri ninaohitaji kuwafuata wale  ambao umeweka kwa uongozi juu yangu. Nitawa shika mkono na kuwa mwaminifu wale unaochagua. Waongoze kwa Roho Wako pia.

*Maandiko ya leo:*

Warumi 8;14; Wote wanaoongozwa na Roho wa MUngu ni watoto wa Mungu.

Hesabu 16:3; nao wakakusanyika kinyume cha Musa na Haruni, na kuwaambia, Ninyi inawatosha, kwa kuwa mkutano wote ni mtakatifu, kila mmoja miongoni mwao,Bwana naye yu kati yao; ni nini basi kujitukuza juu ya mkutano wa Bwana?

## *Maisha yatakuumiza, yakuelimishe, ama yakutie motisha- chaguo ni lako*

Wakati mwingine mambo mabaya huwafanyikia watu wazuri. Wakati Yosefu aliuzwa katika utumwa na akaishi chini ya vile alivyo ota, alikaa na mtazamo mzuri akimngojea Mungu amkomboe. Wakati mambo yalionekana kama hayawezi kubadilika na labda akaona kana kwamba amesahauliwa ndani ya jela la mfalme, Mungu aliendelea kumtendea Yosefu mambo kwa wema. Mpango wa shetani ni kuchukua hali za maisha yako na azitumie kukumaliza wewe na hatima yako. Mungu huchukua hali za maisha yako na kuzitumia kwa kukutengenezea siku za usoni zenye tumaini.

Tunapopitia ugumu wa maisha, lazima tujue kwa utangulizi kuwa shetani anataka yawe kwa ubaya, lakini Mungu ataigeuza iwe kwa uzuri. Usiache maisha yakugandamize. Maisha ni mafupi kugandamizwa kila wakati. Badala yake, wacha maisha yakuelimishe na kukutia motisha kuelekea lengo linalo jalisha… tumaini la Mungu.

### <u>*Ombi la leo:*</u>

Baba, nakuuliza kupitia jina la Yesu uniwezeshe nipite mawimbi ya maisha. Nitakuwa mshindi kupitia kusaidiwa na Wewe na nitaushinda ugumu huu. Maana najua una mpango mkuu wa maisha yangu, Utageuza matatizo yafanyike funzo moja la maisha. Ahsante, Bwana. Amina.

### <u>*Maandiko ya leo:*</u>

2 wakorinitho 4:17-18; Taabu tunayopata ni kidogo, tena ya muda tu: lakini itatupatia utukufu upitao matazamio yote, utukufu ambao hauna mwisho. Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele.

Mwanzo 50:20; nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama livyo leo.

Kutoka1:12; lakini kwa kadiri walivyoteswa, ndivyo walivyo ongezeka na kuzidi kuenea. Nao walichukiwa kwa sababu ya  wana wa Israeli.

## ***Usiwahi ruhusu kile kinafanya kazi juu yako kifanye ndani yako ama itatenda kupitia kwako. Badala yake, wacha Neno la Mungu lifanye kazi ndani yako kuhusu yale yanakutendekeaga  na Mungu atatenda kupitia kwako***

Maisha yanakufanyia kazi sasa hivi. Tangu wakati unapoamka asbuhi hadi  unapoenda kitandani usiku, utaratibu wa dunia hii unajaribu kukushinda wewe. Usipo kasha , misukumo hiyo inayofanya kazi ndani yetu itaingia ndani ya mawazo yetu, yamiliki fikira zetu na yaelekeze hisia zetu. Yote yanayotenda kazi juu yetu yanataka kufanya kazi ndani yetu lili hatimaye yafanye kazi kupitia kwetu na yawaguse watu wengine.

Lazima tuliruhusu Neno la Bwana litende kazi ndani yetu kuhusu yale yanatendeka juu yetu, kisha muumba wa mbingu na nchi  aweza tenda kupitia sisi. Weka maanani kuwa bila maankuli yanayofaa ambayo ni ya Neno la Mungu, filosofia ya ulimwengu yaweza pata mizizi na upate usindi juu yetu.

*Ombi la leo:*

Baba nashukuru kuwa unabadilisha mtazamo wangu kila siku ili uwe sawa na Neno Lako, Mapenzi Yako, na Njia Zako. Mimi ni undongo na wewe ni Mfinyanzi. Neno Lako linapokuwa ndani yangu,wacha litende kazi juu yangu ili ufanye kazi kunipitia mimi. Wacha mapenzi Yako yatendeke maishani mwangu.

*Maandiko ya leo:*

Yohana 16:33; Lakini atakapokuja huyo Roho wa kweli atawaongoza kwenye ukweli wote; maana hatasema kwa mamlaka yake mwenyewe, bali atawaambieni yote atakayosikia, na atasema mambo yatakayokuwa yanakuja.

Yakobo 1:2; Ndugu zangu, muwe na furaha mnapopatwa na majaribu mbalimbali,

1 wathesolenike 2:13; Tunapaswa kumshukuru Mungu daima kwa ajili yenu ninyi ndugu, ninyi mnaopendwa na Bwana, kwa maana Mungu

amewateua tangu mwanzo mpate kuokolewa kwa nguvu ya Roho mfanywe watu wake watakatifu kwa imani yenu katika ukweli.

## *Anapoenda mtu kanisani labda panadhihirisha ni kwa nini yeye huenda kanisani*

Kuna sababu nyingi zinazosababisha watu kuenda kanisani. Wengine huenda kanisani ili wapate vyeo( waimbe kwa kwaya, wafanye kazi ya ofisi, na mambo kama haya)  wengine huenda kanisani kwa mambo ya kibinafsi( wanampenda mhubiri, wanajua marafiki kanisani, na mambo kama haya) wengine huenda ili wajiburudishe. Wanatazamia siku nyingine ya kuenda kucheza na barafu ama kukwea mlima. Hizi zote ni sababu nzuri.

Naamini sababu ile ya maana sana mtu aweza kuchagua kanisa ni kusudi . Kanisa lina kusudi lipi?  Ni kupeleka injili duniani kote? Wakati wako, hazina, na karama ni vitu vya dhamana na lazima ziwekezewe kwa njia ya hekima. Juvhunguze mwenyewe ujue ni kwa nini umeunganishwa na kanisa lako. Kama sababu hizi hazifai, badilisha sababu kabla ubadilishe kanisa.

*Ombi la leo:*

Baba, nisaidie kuchunguza sababu zangu zakuhudhulia kanisa na kama hazilingani na mapenzi Yako, nisaidie ni chunguze tena  na kubadilika vinavyohitajika. Tafadhali bariki kanisa langu ili tuweze Kukupendeza zaidi.

*Maandiko ya leo:*

Matendo ya Mitume 2:47; Walimtukuza Mungu, wakapendwa na watu wote. Kila siku Bwana aliwaongezea idadi ya watu waliokuwa wakiokolewa.

1 Wakorinitho 14:12; Hali kadhalika na ninyi, maadam mna hamu ya kupata vipaji vya Roho, jitahidini hasa kujipatia vile vinavyosaidia kulijenga kanisa.

Waebrania 10:25; Tusiache ile desturi ya kukutana pamoja, kama vile wengine wanavyofanya. Bali tunapaswa kusaidiana kwani, kama mwonavyo, Siku ile ya Bwana inakaribia.

## *Kiti cha mamlaka ndicho chenye usemi wa mwisho*

“maana nilisema hivyo, ndiyo sababu.”

Haya labda ni maneno kila mmoja wetu ameyasikia. Kama watoto ni mara ngapi tuliyasikia maneno haya kutoka kwa wazazi wetu? Mwanzoni wa maisha tulianza kujifunza kuhusu mamlaka na ruhusa. Miaka ilivyoendelea, tukaelewa mamlaka aina nyingi- waalimu, waanjiri, serikali, na wengine kama hawa. Katika njia yetu, twaweza kusikiliza mamlaka haya au tuchague njia yetu ya kibinafsi. Hatimaye, kila mtu lazima anyenyekee chini ya mamlaka, labda kwa uamuzi ama kwa lazima.

Funguo moja ya maisha ambayo yamefaulu na yanatosheleza ni kuelewa kuwa kiti cha mamlaka ndicho kina usemi wa mwisho. Maadiko yanatuambiwa kwamba Mungu ameimarisha mamlaka duniani na pia mbinguni. Kwa hivyo kimsingi tunamtii ama kutomtii Mungu tunapozifuata sheria na mwelekezo za wenye mamlaka juu yetu. Kwa kuwa wafanyi kazi wazuri,na mifano mizuri, kwa hakika tunamheshimu Mungu na kufanyika watoto wazuri wa Baba wa mbinguni.

## *Ombi la leo:*

Baba, nataka kuwa mtoto mzuri na mtiifu Wako. Najua maisha sio kuhusu mimi lakini Wewe. Tafadhali nikumbushe kuwa mamlaka yote hutoka kwako Wewe. Naomba unionyeshe jinsi naweza fanya kazi na amlaka leo kujenga fanaka katika usoni mwangu.

## *Maandiko ya leo:*

Mithali 19:21; waweza fanya mipango mingi, lakini kusudi la Mungu litadumu.

Warumi 13:1-2; Kila mtu anapaswa kuwatii wenye mamlaka katika serikali; maana mamlaka yote hutoka kwa Mungu; nao wenye mamlaka wamewekwa na Mungu. Anayepinga mamlaka ya viongozi anapinga agizo la Mungu; nao wafanyao hivyo wanajiletea hukumu wenyewe.

Chochote usichoweza kuwacha ama uishi bila kitaongoza maisha yako

Kuna wanaume wawili katika Bibilia waliokataa kuwacha kitu walicho kimiliki. Mmoja ni tajiri kijana aliyekuwa mtawala katika Mathayo mtakatifu 19 aliyekuwa na utajiri mwingi na akakataa kuwapa masikini mali yake alipoamurishwa na Yesu. Alijiwekea pesa zake, na akapoteza nafasi yake ya kumfuata Yesu. Wa pili ni mtume Petro, pia katika Mathayo Mtakatifu 19. Petro alisema yeye na wanafunzi wengine

waliwacha kila kitu kufuata Yesu. Kuna tofauti gani kati ya watu hawa wawili? Sio kubwa kwa hakika.

Watu wote hawa wawili walikataa kuachilia kitu walichokuwa wamekidhamini sana. Yule kijana kiongozi mwenye mamlaka alidhamini mali yake kuliko chochote kingine ilhali Petro alidhamini uhusiano wake na Yesu kuliko maisha yenyewe. Chochote ambacho mtu hawezi kuacha ama kuishi bila kitaongoza maisha yake.

## *Ombi la leo:*

Unajua moyo wangu, Bwana. Naomba unionyeshe jinsi yakupanga mambo muhimu zaidi maishani mwangu. Nisaidie kufanya mambo yangu muhimu yafanane na Yako. Nataka kuwa mfano wa maisha yenye utaratibu ambao wengine waweza fuata kwa ujasiri.

## *Maandiko ya leo:*

M athayo Mtakatifu 19:21-22; Yesu akamwambia, "Kama unapenda kuwa mkamilifu, nenda ukauze mali yako uwape maskini hiyo fedha, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate." Huyo kijana aliposikia hayo, aliende zake akiwa mwenye huzuni, maana alikuwa na mali nyingi.

Mathayo Mtakatifu 19:27; Kisha Petro akasema, "Na sisi je? Tumeacha yote tukakufuata; tutapata nini basi?"

Ongeza juu ya usafi wako usiofaa usafi unaofaa

Watu wengi huwazia kuwa ukiwa Mkristo huwezi fanya chochote cha kufurahisha. Mtazamo huu waweza itwa – *usafi usiofaa*- ‘ maana mimi ni Mkristo, siwezi…fanya mambo yakujifurahisha…kama nilivyokuwa nikifanya. Kutofanya mambo mabaya ni njia moja hakika ya kuhufadhi usafi. Hata hivyo kuna zaidi ya uhusiano na Yesu kuliko tu *kuto*fanya mambo mabaya.

Yesu alituambia kuwa ametupa njia tofauti za kutenda mambo- maisha ambayo kwa hakika yanatosheleza. Njia ya maisha yenye furaha ya ukweli ni kutafuta kile mtu aweza kufanya kinachoMfurahisha na kisha ukitende. Hii ni kuongeza usafi unaofaa(kutenda kitu kwa sababu ya Mungu) juu ya usafi wetu usio faa ( kutotenda mambo ambayo yaweza kutomfurahisha). Zaburi 1 hutuambia kuwa mtu ambaye hufikiria jinsi ya kuishi maisha yanayompendeza Mungu humalizia na maisha yenye mazao.

*Ombi la leo:*

Mungu, najua unataka niishi maisha ya furaha na ambayo yanatosheleza. Naomba Bwana, nionyeshe mambo naweza kufanya kutimiza kusudi lile. Nifunze jinsi naweza kuKufurahisha Wewe leo na vile naweza kuwa mfano wakufuatwa na wengine.

*Maandiko ya leo:*

Zaburi 1:1-3; heri mtu yule siyekwenda katika shauri la wasio na haki;wala hakusimama katika njia ya wakosaji; walahakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana, ndiyo impendezayo na sheria Yake huitafakari mchana na usiku; naye atakua kama mti uliopandwa kando kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake; wala jani lake halinyauki na kila atendalo litafaulu.

## ***Badala ya kujenga viwango vyo kupandia, panda juu ya viwango vile***

Wakati mwingine jukumu mbele yetu laweza kuonekana kama lisilowezekana. Nawazia Daudi labda alikuwa na mawazo kama hayo aliposimama mbele ya Goliathi, yule jitu. Labda Nuhu pia aliwazia vivi hivi pia, wakati Mungu alimwambia ajenge safina ambayo ingetumia miaka 100 kabla kumalizika. Yosefu ilimbidi akae na akilenga ndoto yake kwa miaka 25 kabla itimizwe.

Mtu anashinda aje maadui wenye nguvu maishani? Utashida deni, urejeshe ndoa inayoporomoka, ama ushinde vita za madawa ya kulevya? Ni rahisi. Badala ya kujenga viwango vya kupandie, lazima tupande juu ya vile viwango…hatua moja baada ya nyingine. Omba Mungu akupe hatua hiyo nyingine kisha usikae tu pale…ichukue!

*Ombi la leo:*

Baba, ahsante kwamba mimi ni mshindi. Nitawashinda majitu maishani mwangu hatua moja baada ya nyingine. Umeniumba kushinda na kumiliki. Nakushukuru kwamba ninatawala na kuongoza maishani kupitia Yesu Kristo. Leo nitachukua hatua hiyo nyingine.

*Maandiko ya leo:*

Zaburi 37:23;hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, naye aipenda njia yake.

Zaburi 37:31; sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake, hatua zake hazitelezi.

1 Petro 2:21; Hayo ndiyo mliyoitiwa; maana Kristo mwenyewe aliteseka kwa ajili yenu, akawaachieni mfano, ili muufuate mwenendo wake.

## ***Mtu asipojali ninani atanufaika aweza kutenda mambo yasiyo na kiwango***

Kuna motisha nyingi kwa ninini mtu huchagua kufanya yale anyoyafanya. Bahati mbaya ni ngumu kumapata mtu atakayepeana jina lake, karama yake, ama shani yake kutimiza manufaa ya mtu mwingine bila kuhakikisha kwamba wao, kwa njia moja ama nyingine, watapokea manufaa ya mema yaliyotendwa. Wakati mwingi huu hupunguza kiwango cha uzuri ambacho kingeafikiwa kwa sababu hakuna nafasi juu ya jina la mtu Fulani.

Haina kiwango uzuri ambao mtu aweza kutimiza ama kuchangia kama tu aweza wacha kujali ni nani atakayenufaika. Jiulize mwenyewe, ninini kinachokupea motisha kutumia shani yako, wakati wako, ama kufanyiza kazi karama yako ukijaribu kumsaidia mtu mwingine. Unahusika kwa njia kubwa kwa jambo lolote ambalo hutarajii malipo? Kama sivyo, kwa nini usijihusishe?

### *Ombi la leo:*

Mpenzi Mungu, sitaki kuwa aina ya mtu ambaye motisha yake ni ya kujipenda ili apate manufaa ya kibinafsi ama manufaa mengine. Ni nenee na unieleze ni nini ungetaka nijihusishe nacho na nitakutii wewe bila kutarajia malipo.

### *Maandiko ya leo:*

Mathayo Mtakatifu 6:1-5; "Jihadharini msije mkafanya matendo yenu mema mbele ya watu kusudi mwonekane nao. La sivyo, Baba yenu aliye mbinguni hatawapeni tuzo. "Basi, unapomsaidia maskini, usijitangaze. Usifanye kama wanafiki wafanyavyo katika masunagogi na njiani ili watu wawasifu. Kweli nawaambieni, hao wamekwisha pata tuzo lao. Lakini wewe unapomsaidia maskini, fanya hivyo kwamba hata rafiki yako asijue ufanyalo. Toa msaada wako kwa siri, na Baba yako aonaye yaliyofichika, atakutuza. "Mnaposali, msifanye kama wanafiki. Wao hupenda kusimama na kusali katika masunagogi na katika pembe za njia ili watu wawaone. Kweli nawaambieni, hao wamekwisha pata tuzo lao.

## *Usilime kwa punda na ng'ombe wakikokota jembe pamoja*

Bibilia hulinganisha wahuduma wachanga na mambo wanayoweza kwa kazi ya Mungu na ng'ombe ndume. Hawa wanyama hunena kuhusu utegemeaji, nguvu, na uendelezi. Wanakuwa mara nyingi wametosheka na kufurahia kufanya jambo maja kwa kurudia tena na tena, bila kunugunika na vyumbe vya tabia na utaratibu. Punda, kwa upande mwingine,ni wa mwituni na ni ngumu kuwapa elimu yoyote. Pumzi yao inadhuru na wakikuuma wanakuweka viini vibaya. Badala ya kufanya kazi kama kikundi,wao husukuma wenzao ama kumlilia bwana wao na hukataa kutosheka.

Wakiachwa kama wamefunanishwa kwa muda mrefu, punda itamuumiza ngombe ndume na hatimaye iharibu uwezo na upendo wa kuendelea kufanya kazi.labda twafaa kuwa makini wakati wote tunowafunganisha pamoja katuka huduma. 'Usiwahi Lima na ng'ombe na punda wakikokota jembe pamoja.'

### *<u>Ombi la leo:</u>*

Mungu, nipe hekima ninapoitwa kufanya kazi na watu wengine ama ninapepea watu wengine majukumu tofauti. Nisaidie kutoumiza mtu mmoja nikijaribu kumsaidia mwingine katika jina la Yesu, Amina.

### *<u>Maandiko ya leo:</u>*

Kumbukumbu la Torati 22:10; usilime kwa ng'ombe na punda wakikokota jembe pamoja

Mithali 14:4; zizi ni safi ambapo hapana ng'ombe; Bali nguvu za ng'ombe zaleta faida nyingi.

Ayubu 39:5; ni nani aliyempeleka punda- milia aende huru? Au je! Ni nani aliyemfungulia vifungo punda mwitu?